كَيْفِيَّةُ قَضَاءِ الصَّوْمِ

(بَيْنَ التَّتَابُعِ وَالتَّرَاخِيْ)

وَيَلِيْهِ:

حُكْمُ قَضَاءِ الصَّوْمِ عَنِ الْمَيِّتِ

NAMNA YA KULIPA SAUMU/FUNGA

(BAINA YA KUFULULIZA NA KUCHEEWESHA)

NA INAFUATIA:

HUKUMU YA KUMLIPIA SAUMU MAITI

AMEANDIKA:

ABU HALIMA ARAFAT BIN MAHMOUD

UTANGULIZI

Kila sifa njema anastahiki Allaah Mola wa viumbe wote. Swala na salamu zimshukie Mtume Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba.

Ndugu msomaji, kama utakumbuka tuliandika Makala kuhusu Darasa za mwezi wa ramadhani, Makala ambayo tulielezea na kutaja hukumu mbalimbali kuhusiana na mwezi huo, kuanzia fadhila zake mpaka mambo ya swala ya Eid.

Tukumbuke kwamba kuna waislamu waliopatwa na nyudhuru mbalimbali ndani ya mwezi wa ramadhani ambazo ziliwazuia wao kuendelea na kufunga.

Kuna ambao wametimiza idadi ya siku wanazodaiwa na wengine wameshindwa kutimiza ima kwa sababu ya kuendelea kwao na maradhi mpaka wamefikwa na mauti, au walipata nafuu ambayo ingewezakana kwao kulipa lakini wakafanya uzembe mpaka wamefariki, na kundi lingine huwa wanachelewesha kulipa mpaka itawafikia ramadhani nyingine.

Wakati hali ilivyokuwa iko hivyo nikaona niandike Makala hii fupi kufafanua mambo hayo kwa sababu ni miongoni mwa yale ambayo hatuna budi sisi kuyajua, ili tuweze kuwatekelezea maiti wetu yale ambayo yanatupasa sisi kuwafanyia.

Kadhaalika nimeelezea utaratibu wa kulipa baina ya kuharakisha au kuchelewesha, kwa sababu hapo pia kuna uzembe mwingi unaofanywa na watu hasa wanawake.

Mwisho ninasema: Yeyote mwenye rai na maoni au ameona kosa katika yale tuliyoandika namuomba anijulishe kupitia mawasiliano niliyoweka mwisho wa Makala hii, In Shaa Allaah tutapokea kwa mikono miwili na Allaah akulipe kheri.

Ninamuomba Allaah aithibitishe mikono yangu kuandika lililo sawa na aifanye kuwa ni maudhui nyepesi yenye kueleweka.

Wallaahu A’alam.

Ndugu yenu:

Abu Halima Arafat.

Pongwe Tanga.

Tanzania.

Sehemu ya Kwanza: Kuunganisha siku za kulipa saumu

Si wajibu kufululiza kufunga wakati wa kulipa saumu ya ramadhani kwa makubaliano ya Maulamaa wa madhehebu zote nne za ki-fiqhi, na juu ya kauli hiyo kuna kundi kubwa la wanachuoni.

1. **Dalili kutoka kwenye Qur'an ni kauli yake Allaah:**

﴿فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ﴾

"Basi atimize hisabu katika siku nyingine"[1].

Amesema Imam Al-Qurtubi رحمه الله : Amesema Imam Al-Baaji رَحِمَهُ اللهُ :

"وَإِذَا أَتَى بِهَا مُتَفَرِّقَةً فَقَدْ صَامَ عِدَّةً مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ".

"Na akifunga (masiku) hayo kwa kutenganisha atakuwa amefunga katika siku nyingine"[2].

Anakusudia mwenye kulipa saumu ya faradhi kwa kutenganisha atazingatiwa ameifanyia kazi Aya hiyo, kwa sababu maana kutimiza hisabu katika siku nyingine sio maana yake kufululiza na kuunganisha wakati kulipa, hapana.

2. **Athari ya Ibn Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا :**

Amesema Ibn Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا akifafanua aya iliyotangulia:

" لاَ بَأْسَ أَنْ يُفَرَّقَ".

"Hapana ubaya kutenganisha"[3].

****

[1]- Surat Al-Baqara/184.
[2]- Tafsiirul Qurtubi (Jz. 2, Uk. 282).
[3]- Ameitaja Bukhari kwa taaliq kwa tamko la jazmi na ameifanyia waslu Ibn Hajar katika: [At taghliiq].

SEHEMU YA PILI: Kuchelewesha kulipa

Nukta ya kwanza: Kuchelewesha kulipa siku alizoacha kufunga katika mwezi wa ramadhani, lakini akafunga kabla haijaingia ramadhani nyingine:

Inafaa mtu kulipa kwa kuchelewesha siku alizoacha kufunga katika mwezi wa ramadhani, kwa hiyo anaruhusiwa kulipa kuanzia mwezi wa shawwaal mpaka sha'bani muda wa kuwa hazijabaki katika mwezi wa sha'bani siku ambazo zinalingana na siku anazotakiwa kulipa, hapo atalazimika kufululiza, hilo ni kwa makubaliano ya maimamu wa madhehebu zote nne.

Kauli ya Ibn Hajar na Imam Nnawawi kuhusu jambo hili:

Amesema Ibn Hajar رَحِمَهُ اللهُ :

"ظَاهِرُ صَنِيْعِ الْبُخَارِيِّ يَقْتَضِيْ جَوَازَ التَّرَاخِيْ وَالتَّفْرِيْقِ... وَهُوَ قَوْلُ الْجُمْهُوْرِ".

"Dhahiri ya mpangilio wa Bukhari unahukumilia kwenye kujuzu kuchelewesha na kutenganisha (siku za kulipa) na hiyo ndio kauli ya Jumhuri (kundi kubwa la wanachuoni)"[4].

Na amesema Imam Nnawawi رَحِمَهُ اللهُ :

"إِذَا لَزِمَهُ قَضَاءُ رَمَضَانَ أَوْ بَعْضُهُ فَإِنْ كَانَ فَوَاتُهُ بِعُذْرٍ كَحَيْضٍ وَنِفَاسٍ... فَقَضَاؤُهُ عَلَى التَّرَاخِي بِلَا خِلَافٍ مَا لَمْ يَبْلُغْ بِهِ رَمَضَانَ الْمُسْتَقْبَلِ وَلَكِنْ يُسْتَحَبُّ تَعْجِيلُهُ".

"Mtu ikimlazimu yeye kulipa ramadhani yote au baadhi yake, ikiwa kumpita kwake (masiku hayo) kwa sababu ya udhuru kama vile Hedhi na Nifasi... basi (inajuzu) kuilipa kwake kwa kuchelewesha bila khilafu yoyote, muda wa kuwa hakufikia katika kulipa kwake ramadhani inayofuata, lakini inapendekezwa kuharakisha (kulipa)"[5].

3. **Dalili katika sunnah:**

«كَانَ يَكُونُ عَلَيَّ الصَّوْمُ مِنْ رَمَضَانَ، فَمَا أَسْتَطِيعُ أَنْ أَقْضِيَهُ إِلَّا فِي شَعْبَانَ، الشُّغْلُ مِنْ رَسُولِ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، أَوْ بِرَسُولِ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ».

"Ilikuwa jambo lilivyo kunawajibika juu yangu kulipa saumu ya ramadhani, nashindwa kulipa isipokuwa katika mwezi wa sha'bani, kinachonizuia ni shughuli kwa ajili ya kumtumikia Mtume ﷺ au kwa sababu ya Mtume ﷺ "[6].

4- Fat-hul baari (Jz. 4, Uk. 189).
5- Al-Majmuu' (Jz. 6, Uk. 365).
6- Bukhari (1950) na Muslim (1146).

Nukta ya Pili: Kuchelewesha kulipa siku ulizoacha kufunga katika mwezi wa ramadhani bila udhuru wowote wa kisheria mpaka ikaingia ramadhani nyingine:

Kuna kauli mbili za wanachuoni juu ya mtu aliyechelewesha kulipa siku za ramadhani mpaka ikafika ramadhani nyingine:

Kauli ya kwanza: Itamlazimu yeye kulipa siku zilizompita pamoja na kutoa fidia, ambayo ni kumlisha masikini mmoja kila siku kwa idadi ya siku hizo.

Amesema Imam Nnawawi رَحِمَهُ‌اللهُ :

"وَإِنْ كَانَ لِغَيْرِ عُذْرٍ، فَعَلَيْهِ مَعَ الْقَضَاءِ إِطْعَامُ مِسْكِينٍ لِكُلِّ يَوْمٍ. وَبِهَذَا قَالَ ابْنُ عَبَّاسٍ، وَابْنُ عُمَرَ، وَأَبُو هُرَيْرَةَ، وَمُجَاهِدٌ، وَسَعِيدُ بْنُ جُبَيْرٍ، وَمَالِكٌ، وَالثَّوْرِيُّ، وَالْأَوْزَاعِيُّ، وَالشَّافِعِيُّ، وَإِسْحَاقُ".

"Ikiwa (amechelewesha) bila ya udhuru wowote, itapasa juu yake pamoja na kulipa (saumu) alishe masikini mmoja kila siku. Na kwa kauli hii amesema Ibn Abbas, Ibn Umar, Abu Huraira, Mujahid, Said Bin Jubair, Malik, At-Thauri, Al-Auzaai', Shafi' na Is-haaq"[7].

Ama kuhusiana na kiwango unachotakiwa kumlisha masikini mmoja ni nusu ya pishi, ambayo ni sawa na kilo moja na robo kwa vipimo vyetu vya kisasa.

Je ni kiwango gani cha fidia kwa mtu ambaye amechelewesha kulipa bila ya udhuru wowote mpaka zikamdiriki yeye ramadhani mbili na zaidi?

Kundi kubwa la Maulamaa wa madhehebu ya imam Malik, Ahmad na Shafi' wanaona kwamba fidia haiongezeki, kwa hiyo mtu ambaye amechelewesha kulipa hata kama ni miaka mingi si lazima juu yake kutoa fidia ya kila mwaka ambao amechelewesha kulipa na badala yake itamlazimu yeye kutoa fidia mara moja tu.

Amesema Imam Nnawawi رَحِمَهُ‌اللهُ :

"فَإِنْ أَخَّرَهُ لِغَيْرِ عُذْرٍ حَتَّى أَدْرَكَهُ رَمَضَانَانِ أَوْ أَكْثَرُ، لَمْ يَكُنْ عَلَيْهِ أَكْثَرُ مِنْ فِدْيَةٍ مَعَ الْقَضَاءِ؛ لِأَنَّ كَثْرَةَ التَّأْخِيرِ لَا يَزْدَادُ بِهَا الْوَاجِبُ".

"Na akichelewesha (kulipa) bila ya udhuru wowote mpaka zikamdiriki yeye ramadhani mbili au zaidi, haipasi juu yake zaidi ya kutoa fidia moja (tu) pamoja na kulipa (siku zote alizoacha). Kwa sababu wajibu (wa kutoa fidia hautazidi kwa ajili ya wingi wa siku za kuchelewesha (kulipa)"[8].

7- Al-Mughni (Jz. 3, Uk. 153).
8- Al-Mughni (Jz. 3, Uk. 154).

Lakini kauli iliyo sahhihi zaidi katika madhehebu ya Imam Shafi' ni kwamba fidia inazidi kwa kuongezeka siku ulizoacha kulipa.

Amesema Imam Nnawawi رَحِمَهُ‌اللهُ :

"وَلَوْ أَخَّرَهُ حَتَّى مَضَى رَمَضَانَانِ فَصَاعِدًا فَهَلْ يَتَكَرَّرُ عَنْ كُلِّ يَوْمٍ بِتَكَرُّرِ السِّنِينَ أَمْ يَكْفِي مُدٌّ عَنْ كُلِّ السِّنِينَ فِيهِ وَجْهَانِ مَشْهُورَانِ ذَكَرَهُمَا الْمُصَنِّفُ بِدَلِيلِهِمَا (أَصَحُّهُمَا) يَتَكَرَّرُ صَحَّحَهُ إمَامُ الْحَرَمَيْنِ وَغَيْرُهُ وَقَطَعَ بِهِ الْقَاضِي أَبُو الطَّيِّبِ فِي كِتَابِهِ الْمُجَرَّدِ وَخَالَفَهُمْ صَاحِبُ الْحَاوِي فَقَالَ الْأَصَحُّ أَنَّهُ يَكْفِي مُدٌّ وَاحِدٌ لِجَمِيعِ السِّنِينَ وَالْأَوَّلُ أَصَحُّ".

"Lau alicheleweshа (kulipa) mpaka zikapita ramadhani mbili au zaidi, je itaongezeka (fidia ya) kila siku kwa kuzingatia kwa sababu ya kujirudia miaka au kibaba kimoja kinatosha kwa miaka yote? Katika hili kuna njia mbili zilizo mashuhuri ambazo amezitaja Mtunzi kwa dalili zake, iliyo sahihi zaidi ni (kwamba) itaongezeka (fidia kila mwaka), ameisahihisha kauli hiyo imamul Haramain (Al-Juwain) na wengine, na Qadhi Abu Ttwayyib katika amekata kauli (juu ya msimamo huo) kwenye kitabu chake Al-Mujarrad. Ama mwenye kitabu Al-Haawi yeye ametafautiana na (wanachuoni) hao, amesema: kauli sahihi zaidi ni kwamba kibaba kimoja kinatosheleza (fidia) kwa miaka yote, na kauli ya kwanza ndio sahihi zaidi"[9].

Pia amesema tena kuhusu mtu aliyekula mchana wa ramadhani kwa jeuri na dhulma:

"وَلَوْ أَفْطَرَ عُدْوَانًا وَقُلْنَا تَجِبُ فِيهِ الْفِدْيَةُ فَأَخَّرَ الْقَضَاءَ حَتَّى دَخَلَ رَمَضَانُ آخَرُ فَعَلَيْهِ لِكُلِّ يَوْمٍ مَعَ الْقَضَاءِ فِدْيَتَانِ فِدْيَةٌ لِلْإِفْطَارِ عُدْوَانًا وَأُخْرَى لِلتَّأْخِيرِ هَذَا هُوَ الْمَذْهَبُ وَبِهِ قَطَعَ الْبَغَوِيُّ وَغَيْرُهُ"

"Na lau alikula kwa dhulma na tumesema kwamba atatoa fidia, kisha akachelewesha kulipa mpaka ikaingia ramadhani nyingine, basi italazimu juu yake kulipa siku zote pamoja na kutoa fidia mara mbili, fidia moja kwa ajili ya kula mchana (wa ramadhani) kwa jeuri na dhulma na fidia nyingine kwa ajili ya kuchelewesha, hii ndio kauli (ya kutegemewa) katika madhehebu (ya imamu Shafi') na kwa kauli hii amesema kwa kukata imamu Al-Baghwi na Maulamaa wengine"[10].

Kauli ya Pili: Haitamlazimu yeye isipokuwa kufunga tu (hakuna kutoa fidia). Haya ndio madhehebu ya Abu Hanifa na ndio kauli aliyoichagua Ibn Hazmi, As shaukani na Ibn Uthaimin رَحِمَهُمُ اللهُ :

9- Al-Majmuu' (Jz. 6, Uk. 364).
10- Al-Majmuu' (Jz. 6, Uk. 364).

Amesema Ibn Hazmi رَحِمَهُ‌اللهُ :

"وَمَنْ كَانَتْ عَلَيْهِ أَيَّامٌ مِنْ رَمَضَانَ فَأَخَّرَ قَضَاءَهَا عَمْدًا، أَوْ لِعُذْرٍ، أَوْ لِنِسْيَانٍ حَتَّى جَاءَ رَمَضَانُ آخَرُ فَإِنَّهُ يَصُومُ رَمَضَانَ الَّذِي وَرَدَ عَلَيْهِ كَمَا أَمَرَهُ اللَّهُ تَعَالَى فَإِذَا أَفْطَرَ فِي أَوَّلِ شَوَّالٍ قَضَى الْأَيَّامَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِ وَلَا مَزِيدَ، وَلَا إطْعَامَ عَلَيْهِ فِي ذَلِكَ؛ وَكَذَلِكَ لَوْ أَخَّرَهَا عِدَّةَ سِنِينَ وَلَا فَرْقَ إلَّا أَنَّهُ قَدْ أَسَاءَ فِي تَأْخِيرِهَا عَمْدًا".

“Yule ambaye anadaiwa masiku ya ramadhani, kisha akachelewesha kulipa kwake kwa makusudi, kusahau au kwa sababu ya udhuru, mpaka ikaingia ramadhani nyingine, basi atafunga ile ramadhani iliyomfikia kama alivyo amrishwa na Allaah Ta’alaa, atakapofungua katika mwezi wa shawwaal atalipa siku zilizo wajibu juu yake wala hapana kuzidisha (chochote), wala haimpasi yeye katika hilo kulisha (masikini), na hivyo hivyo lau kama alicheleweshe (kulipa) kwa miaka mingi hakuna tafauti, (atalipa funga tu wala hatolisha masikini), isipokuwa atakuwa amefanya dhambi kwa kuchelewesha kwake hali ya kukusudia”[(11)].

Amesema Imamu As sahukani رَحِمَهُ‌اللهُ :

"وَقَدْ بَيَّنَّا أَنَّهُ لَمْ يَثْبُتْ فِي ذَلِكَ عَنْ النَّبِيِّ - صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - شَيْءٌ، وَأَقْوَالُ الصَّحَابَةِ لَا حُجَّةَ فِيهَا، وَذَهَابُ الْجُمْهُورِ إلَى قَوْلٍ لَا يَدُلُّ عَلَى أَنَّهُ الْحَقُّ"

“Hakika tumekwisha bainisha ya kwamba haijathibiti hadithi yoyote kutoka kwa Mtume ﷺ kuhusu jambo hilo, na kauli za Maswahaba katika hilo si hoja, na Jumhuri (kundi kubwa la wanachuoni) kuifanyia kazi kwao kauli fulani haifahamishi kuwa hiyo ndio haki”[(12)].

Amesema sheikh Ibn Uthaimin رَحِمَهُ‌اللهُ :

"إذَا تَرَكَ الْإِنْسَانُ قَضَاءَ رَمَضَانَ إلَى رَمَضَانِ الثَّانِي بِلَا عُذْرٍ فَهُوَ آثِمٌ وَعَلَيْهِ أَنْ يَقْضِيَ مَا فَاتَهُ وَلَا إطْعَامَ عَلَيْهِ عَلَى الْقَوْلِ الصَّحِيحِ

“Pindi mtu akiacha kulipa (siku anazodaiwa) katika ramadhani bila ya udhuru wowote mpaka ikaingia ramdhani ya pili, atapata madhambi na ni wajibu juu yake kulipa (siku) zilizompita, wala si wajibu kwake kulisha (masikini) kwa kauli iliyo sahihi”[(13)].

Hoja yao ni kwamba, Aya imezungumzia kulipa tu siku zilizokupita katika ramadhani wala haikutaja fidia, kwa hiyo litabakia lile ambalo limetajwa ndani ya Aya, ambalo ni kulipa kwa kufunga siku ulizoacha katika ramadhani si kulipa fidia.

11- Al-Muhallaa (Jz. 4, Uk. 407).
12- Nailul Autwaari (Jz. 4, Uk. 278).
13- Majmuu fataawa warasaail Ibn Uthaimin (Jz. 19, Uk. 385).

NUKTA YA TATU: Hukumu ya kufunga sunnah kabla ya kulipa saumu ya faradhi

Kuna walioruhusu katika wanachuoni na wengine wanaona kuwa ni karaha kutanguliza kufunga sunna kabla ya kutimza hesabu ya saumu ya faradhi.

Amesema Ibn ‘Aabidiin رَحِمَهُ اللهُ :

"وَلَوْ كَانَ الْوُجُوْبُ عَلَى الْفَوْرِ لَكُرِهَ لِأَنَّهُ يَكُوْنُ تَأْخِيْرًا لِلْوَاجِبِ عَنْ وَقْتِهِ الْمُضَيَّقِ"

“Lau ingelikuwa (kulipa) ni wajibu unaopasa kutekelezwa kwa haraka ingelikuwa ni karaha (kufunga sunnah kabla ya kulipa faradhi), kwa sababu itakuwa ni kuucheleesha wajibu (na) kuutoa nje ya muda wake uliodhiki”[14].

Maneno haya maana yake ni kuwa inafaa kufunga sunna kabla ya kulipa funga ya ramadhani na wala sio karaha, kwa sababu muda wa kulipa ni mrefu.

Amesema Sheikh Ibn Uthaimin رَحِمَهُ اللهُ:

"لَا شَكَّ أَنَّهُ مِنَ الْمَشْرُوْعِ وَالْمَعْقُوْلِ أَنْ يَبْدَأَ بِالْفَرِيْضَةِ قَبْلَ النَّافِلَةِ، لِأَنَّ الْفَرِيْضَةَ دَيْنٌ وَاجِبٌ عَلَيْهِ، وَالنَّافِلَةَ تَطَوُّعٌ إِنْ تَيَسَّرَتْ وَإِلَّا فَلَا حَرَجَ، وَعَلَى هَذَا فَنَقُوْلُ لِمَنْ عَلَيْهِ قَضَاءٌ مِنْ رَمَضَانَ: اِقْضِ مَا عَلَيْكَ قَبْلَ أَنْ تَتَطَوَّعَ، فَإِنْ تَطَوَّعَ قَبْلَ أَنْ يَقْضِيَ مَا عَلَيْهِ فَالصَّحِيْحُ أَنَّ صِيَامَهُ التَّطَوُّعَ صَحِيْحٌ مَا دَامَ فِي الْوَقْتِ سَعَةٌ، لِأَنَّ قَضَاءَ رَمَضَانَ يَمْتَدُّ إِلَى أَنْ يَكُوْنَ بَيْنَ الرَّجُلِ وَبَيْنَ رَمَضَانَ الثَّانِيْ مِقْدَارُ مَا عَلَيْهِ، فَمَا دَامَ الْأَمْرُ مُوَسَّعاً فَالنَّفْلُ جَائِزٌ... هَذَا بِالنِّسْبَةِ لِصَوْمِ التَّطَوُّعِ الْمُطْلَقِ الَّذِيْ لَا يَرْتَبِطُ بِرَمَضَانَ".

“Hapana shaka kisheria na kiakili ya kuwa aanze na (ibada ya) faradhi kabla ya sunna, kwa sababu faradhi ni deni la wajibu juu yake, na sunna ni utiifu wa kujitolea ikiwa ni wepesi (atafanya) na akishindwa hapana ubaya, na juu ya msingi huu tunasema kumwambia yule ambaye ana juu yake siku za kulipa katika ramadhani: lipa (kwanza) siku unazodaiwa kabla hujafunga sunna, na ikiwa atafunga sunna kabla hajalipa siku za ramadhani iliyo sahihi ni kwamba funga yake ya sunna iko sahihi, muda wa kuwa kuna wasaa (katika wakati wa kulipa), kwa sababu muda wa kulipa saumu ya ramadhani unarefuka mpaka inakuwa (muda uliobaki) baina ya mtu na kuingia ramadhani ya pili ni kiasi cha siku anazodaiwa (hapo ni wajibu wake kufululiza), kwa hiyo muda wa kuwa jambo hilo ni lenye wasaa basi inajuzu kufunga sunna... (lakini) hilo ni kwa kuzingatia funga ya sunna Mutlaq (haina mafungamana na ramadhani, kama vile Jumatatu, Al-Khamis, Arafa n.k).

Kisha akafafanua vizuri na kubainisha ni funga ili ya sunna ataruhusiwa mtu kuifunga kabla ya kulipa siku za ramadhani na sun api hatafunga mpaka akamilishe kulipa.

[14]- Haashiyat Ibn Aabidiin (Jz. 4, Uk. 423).

"أَمَّا صِيَامُ سِتَّةِ أَيَّامٍ مِنْ شَوَّالٍ فَإِنَّهَا مُرْتَبِطَةٌ بِرَمَضَانَ وَلَا تَكُوْنُ إِلَّا بَعْدَ قَضَائِهِ، فَلَوْ صَامَهَا قَبْلَ الْقَضَاءِ لَمْ يَحْصُلْ عَلَى أَجْرِهَا، ... بَعْضُ النَّاسِ أَنَّهُ إِذَا خَافَ خُرُوْجَ شَوَّالٍ قَبْلَ صَوْمِ السِّتِّ فَإِنَّهُ يَصُوْمُهَا وَلَوْ بَقِيَ عَلَيْهِ الْقَضَاءُ، وَهَذَا غَلَطٌ فَإِنَّ هَذِهِ السِّتَّةَ لَا تُصَامُ إِلَّا إِذَا أَكْمَلَ الْإِنْسَانُ مَا عَلَيْهِ مِنْ رَمَضَانَ".

“Ama saumu ya siku sita za shawwaal (siku) hizo zinafungamana na ramadhani na wala hazifungwi mpaka baada ya kulipa (ramadhani), lau mtu alifunga (sita shawwaal) kabla ya kukamilisha kulipa (ramadhani) hatopata ujira wake... baadhi ya watu akihofia kumalizika kwa mwezi wa shawwaal kabla hajafunga siku sita basi yeye anafunga hata kama zimebaki (siku) za kulipa, haya ni makosa, kwa sababu hizi siku sita hazifungwi isipokuwa akikamilisha mtu (funga ya) ramadhani”[15].

****

SEHEMU YA TATU: Kufunga kwa ajili ya maiti aliyecheleweshe kulipa kwa sababu ya udhuru

Mtu amecheleweshe kulipa saumu/funga ya wajibu mfano: ramadhani, nadhiri, kafara n.k, kwa sababu udhuru mpaka amefariki, hadaiwi chochote, si kufunga wala kulisha masikini, kwa makubaliano ya Maulamaa wa madhehebu zote nne.

Amesema Imamu Nnawawi رَحِمَهُ اللهُ :

"{فَرْعٌ} فِي مَذَاهِبِ الْعُلَمَاءِ فِيمَنْ مَاتَ وَعَلَيْهِ صَوْمٌ فَاتَهُ بِمَرَضٍ أَوْ سَفَرٍ أَوْ غَيْرِهِمَا مِنْ الْأَعْذَارِ وَلَمْ يَتَمَكَّنْ مِنْ قَضَائِهِ حَتَّى مَاتَ. ذَكَرْنَا أَنَّ مَذْهَبَنَا أَنَّهُ لَا شَيْءَ عَلَيْهِ وَلَا يُصَامُ عَنْهُ وَلَا يُطْعَمُ عَنْهُ بِلَا خِلَافٍ عِنْدَنَا وَبِهِ قَالَ أَبُو حَنِيفَةَ وَمَالِكٌ وَالْجُمْهُورُ قَالَ الْعَبْدَرِيُّ وَهُوَ قَوْلُ الْعُلَمَاءِ كَافَّةً إِلَّا طَاوُسًا وَقَتَادَةَ فَقَالَا يَجِبُ أَنْ يُطْعَمَ عَنْهُ لِكُلِّ يَوْمٍ مِسْكِينٌ لِأَنَّهُ عَاجِزٌ فَأَشْبَهَ الشَّيْخَ الْهَرِمَ"

“Hii ni tanzu: katika kuelezea madhehebu ya Maulamaa kuhusiana na mtu aliyekufa akiwa anadaiwa saumu ya wajibu ambayo hakufunga kwa sababu ya maradhi, safari au udhuru mwingine kisha hakuweza kulipa mpaka amekufa. Tumetaja kwamba hakuna khilafu yoyote katika madhehebu yetu kuwa (mtu huyo) hakuna kitu chochote juu yake (hadaiwi kitu), hapafungwi wala kulisha chakula (fidia) kwa ajili yake, na kwa kauli hiyo amesema (pia) Abu Hanifa, Malik, na Jumhuri (kundi kubwa la Maulamaa), amesema Al-‘Abdariy: na hiyo ndio kauli ya Maulamaa wote isipokuwa Twaaus na Qatada (wao) wamesema ni wajibu kulisha chakula kwa masikini mmoja kila siku kwa ajili yake, kwa sababu yeye ni mwenye kushindwa kwa hiyo akafanana na mzee mtu mzima (asiyeweza kunga)”[16].

****

[15]- Majmuul fataawa warasaaili Ibn Uthaimin (Jz. 20, Uk. 49).
[16]- All-Majmuu’ (Jz. 6, Uk. 372).

SEHEMU YA NNE: Kufunga kwa niaba ya maiti ambaye amecheleweshа kulipa bila ya udhuru wowote

Mtu amekufa akiwa anadaiwa funga ya wajibu kama ilivyotangulia, lakini alipopata wasaa hakulipa, alifanya uzembe mpaka amefariki, inapasa kwa walii wake (mrithi wake) kufunga kwa niaba yake siku zote alizoacha, na kama hakuweza basi alishe kila siku masikini mmoja. Hayo ndio madhehebu ya Imamu Shafi kwa kauli yake ya zamani (Qadiim), na ameichagua kauli hiyo Imamu Nnawawi, Ibn Baaz na Ibn Uthaimin رَحِمَهُمُ اللهُ na dalili yao ni hadithi ya Aisha رَضِيَ اللهُ عنها inayosema:

«مَنْ مَاتَ وَعَلَيْهِ صِيَامٌ صَامَ عَنْهُ وَلِيُّهُ»

"Ataekufa na anadaiwa saumu (ya wajibu) basi afunge walii wake kwa niaba yake"[17].

Amesema Sheikh Ibn Baaz رَحِمَهُ اللهُ wakati akielezea maana ya hadithi hii:

"أَنَّ الصَّوْمَ يُقْضَى عَنِ الْمَيِّتِ، سَوَاءٌ كَانَ نَذْرًا أَوْ صَوْمَ رَمَضَانَ أَوْ صَوْمَ كَفَّارَةٍ فِيْ أَصَحِّ أَقْوَالِ أَهْلِ الْعِلْمِ، وَإِنْ لَمْ يَتَيَسَّرِ الْقَضَاءُ أَطْعَمَ عَنْ كُلِّ يَوْمٍ مِسْكِيْنًا، هَذَا كُلُّهُ إِذَا كَانَ الَّذِيْ عَلَيْهِ الصِّيَامُ قَصَّرَ فِيْ الْقَضَاءِ وَتَسَاهَلَ، أَمَّا إِذَا كَانَ مَعْذُوْرًا بِمَرَضٍ أَوْ نَحْوِهِ مِنَ الْأَعْذَارِ الشَّرْعِيَّةِ، فَلَا إِطْعَامَ وَلَا صِيَامَ عَلَى الْوَرَثَةِ".

"Katika kauli iliyo sahihi zaidi miongoni mwa kauli za Maulamaa ni kwamba maiti analipiwa saumu/funga, sawa imekuwa ni funga ya nadhiri, ramadhani au kafara, na ikiwa haikuwa wepesi kwake kulipa atalisha kila siku masikini mmoja, haya yote ni pale itakapokuwa yule ambaye anawajibika kufunga alizembea katika kulipa na akapuuza. Ama akiwa ni mwenye udhuru wa maradhi n.k. miongoni mwa nyudhuru za kisheria, basi hapana kwa warithi wake kufunga wala kulisha (masikini)"[18].

Amesema Imamu Nnawawi رَحِمَهُ اللهُ :

"(وَالْقَوْلُ الثَّانِيْ) وَهُوَ الْقَدِيْمُ أَنَّهُ يَجُوْزُ لِوَلِيِّهِ أَنْ يَصُوْمَ عَنْهُ وَلَا يَلْزَمُهُ ذَلِكَ وَعَلَى هَذَا الْقَوْلِ لَوْ أَطْعَمَ عَنْهُ جَازَ فَهُوَ عَلَى الْقَدِيْمِ مُخَيَّرٌ بَيْنَ الصِّيَامِ وَالْإِطْعَامِ ... وَهَذَا الْقَدِيْمُ هُوَ الصَّحِيحُ عِنْدَ جَمَاعَةٍ مِنْ مُحَقِّقِي أَصْحَابِنَا الْجَامِعِينَ بَيْنَ الْفِقْهِ وَالْحَدِيْثِ".

"Na kauli ya Pili: nayo ni kauli ya zamani (qadiim), inajuzu kwa walii wake kufunga kwa niaba yake na wala haimlazimu, na juu ya kauli hii, lau kama atalisha tu itafaa, na kwa kauli hiyo ya zamani (qadiim) walii amepewa hiyari/kuchagua baina ya kufunga au kulisha maskini, na hii kauli hii ndio sahihi mbele ya Maulamaa wetu wengi wenye kuhakiki mambo, waliokusanya baina ya Fiqh na Hadithi."[19].

[17]- Bukhari (1952) na Muslim (1147)
[18]- Majmuu' fataawa Ibn Baaz (Jz. 15, Uk. 372).
[19]- Al-Majmuu' sharhil muhaddhab (Jz. 5, Uk. 363).

Amesema Al-Khatib As- Sharbiini رَحِمَهُ‌اللهُ :

"وَفِي الْقَدِيمِ: يَصُومُ عَنْهُ وَلِيُّهُ - أَيْ يَجُوزُ لَهُ الصَّوْمُ عَنْهُ - بَلْ يُنْدَبُ لَهُ، وَيَجُوزُ لَهُ الْإِطْعَامُ"

“Na kauli ya zamani (Qadiim – inasema) walii wake atafunga kwa niaba yake, maana yake: inajuzu kwa (walii) kufunga kwa niaba yake bali inapendekezwa kwake, na (pia) inajuzu kwake kulisha masikini (badala ya kufunga)”[20].

Amesema Sheikh Ibn Uthaimin رَحِمَهُ‌اللهُ :

"إِذَا كَانَ رَجُلٌ قَدْ أَفْطَرَ فِيْ رَمَضَانَ لِسَفَرٍ أَوْ لِمَرَضٍ ثُمَّ عَافَاهُ اللهُ مِنَ الْمَرَضِ وَلَمْ يَصُمِ القَضَاءَ الَّذِيْ عَلَيْهِ ثُمَّ مَاتَ، فَإِنَّ وَلِيَّهُ يَصُوْمُ عَنْهُ، سَوَاءٌ كَانَ ابْنَهُ، أَوْ أَبَاهُ، أَوْ أُمَّهُ، أَوِ ابْنَتَهُ، المُهِمُّ أَنْ يَكُوْنَ مِنَ الْوَرَثَةِ، وَإِنْ تَبَرَّعَ أَحَدٌ غَيْرُ الْوَرَثَةِ فَلَا حَرَجَ أَيْضاً، وَإِن لَّمْ يَقُمْ أَحَدٌ بِالصِّيَامِ عَنْهُ فَإِنَّهُ يُطْعِمُ مِنْ تَرِكَتِهِ لِكُلِّ يَوْمٍ مِسْكِيْناً.

“Ikiwa mtu amekula (mchana wa) ramadhani kwa ajili ya safari au maradhi, kisha Allaah akamponya na maradhi hayo na wala hakufunga siku anazodaiwa mpaka amekufa, basi walii wake afunge kwa ajili yake, ni sawa awe mtoto wake wa kiume, baba yake, mama yake au binti yake, muhimu awe ni katika warithi (wake), na akijitolea (kufunga) asiyekuwa mrithi pia hapana vibaya, na kama hakuna yeyote aliyefunga kwa ajili yake basi alishe kila siku masikini mmoja kutoka kwenye mali aliyoiacha”[21].

****

Namuomba Allaah aniruzuku Ikhlaas katika kauli na matendo na aweke qabuli katika amali yangu hii ilete manufaa kwa waja wake na anisamehe madhambi yangu, mimi wazazi wangu na waislamu wote, hakika yeye juu ya kila kitu ni Muweza.

Abu Halima Arafat
Ijumaa/5/shawwaal/1443M – 06/05/2022H
Pongwe Tanga.
Simu: 0715263253
shayhat033@gmail.com

[20]- Mughnil muhtaaj (Jz. 1, Uk. 172).
[21]- Majmuu’ fataawa warasaaili Ibn Uthaymin (Jz. 15, Uk. 395).